

**Usiaji wa mbegu**

- Sia pakiti yenye gramu 3 kwenye tuta lenye ukubwa wa sentimita za eneo 30.
- Sia mbegu asubuhi na mapema au jioni ili kuzuia madhara yaletwayo na upepo.

**Njia ya usiaji**

- Gawanya pakiti ya mbegu katika sehemu 3 zinazolingana
- Pakiti ya gramu 3 inashauriwa katika kila tuta
- Sia keni tatu za maji kwa kila tuta (1/3) ya pakiti ya mbegu





*Utunzaji wa kitalu kabla ya miche kuota*


KWA MAWASILIANO :

TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU

TANZANIA (TORITA)

S.L.P 431,

TABORA.

Barua pepe : info@torita.or.tz

Tovuti:*www.torita.or..tz*


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO
CHAKULA NA USHIRIKA**

**TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU
TANZANIA (TORITA)**



# *UTUNZAJI SAHIHI WA VITALU*

**UANDAAJI NA UTUNZAJI SAHIHI WA VITALU (UWEKAJI WA MBOLEA NA USIAJI)**

**Uandaaji na utunzaji sahihi wa vitalu**

**Madhumuni**

- Kuinua matumizi sahihi ya teknolojia katika uandaaji wa vitalu
- Kusisitiza matumizi sahihi ya vitalu visafi
- Kuinua usiaji sahihi wa mbegu vitaluni ili kupata miche yenye afya na inayolingana

**Uchaguzi wa eneo la kitalu**

- Liwe na maji safi ya kutosha umwagiliaji wa kitalu na pawe na wigo kuzuia watu na wanyama wasiweze kuchafua maji yaliyomo.
- Lisiwe linaruhusu maji kusimama na mwinuko wake usizidi asilimia kumi.
- Liwe karibu na unapoishi ili lihudumiwe kwa urahisi, lakini liwe mbali na mabani kuzuia magonjwa ya tumbaku kitaluni.
- Liwe na udongo wenye rutuba ya kutosha, unapopitisha hewa kwa urahisi na haupotezi unyevu unyevu haraka.
- Pawe hapajalimwa tumbaku au mimea mingine ya jamii ya tumbaku kama vile nyanya au bilinganya kwa kipindi kisichopungua miaka mitatau.
- Epuka eneo linaloweza kuleta kivuli kwenye miche kitaluni.

**Ukubwa wa tuta**

- Liwe na upana wa mita 1.5 na urefu wa mita 20.
- Ukubwa huu unashauriwa kwa ajili ya kurahisisha utunzaji wa vitalu.
- Matuta matatu yanatosha kutoa miche ya hekta moja.

**Ulimaji wa matuta ya kitalu**

- Andaa eneo mapema wakati udongo ukiwa na unyevu hii itawezesha masalia ya mimea kuoza vizuri.
- Lima eneo ili kuwezesha hewa na maji kupita vizuri na ukuaji



**Utunzaji wa kitalu kabla ya kumwagilia**

**Madhumuni:**

- Kuinua kiwango cha unyevu kabla ya kusia mbegu.
- Kuotesha magugu ili kuzuia miche kushindana na magugu katika kupata virutubisho.

**Njia:**

- Panga nyasi juu ya matuta kabla ya kumwagilia.
- Nyasi ziwe ni zile zenye mashina manene na majani kidogo
- Mwagilia kila siku juu ya nyasi siku 15 kabla ya kusia mbegu.
- Wek… siku



**Uandaaji wa kitalu kabla ya kusia**

- Usisimame juu ya tuta wakati unafanya kazi kwani tuta bado lina unyevu.
- Ondoa nyasi juu ya tuta.
- Saw… …ba mabonde taya…



**Uwekaji wa mbolea**

- Tawanya kilo 5 za NPK kwa kila tuta.
- Gawanya tuta katika sehemu 5 zinazolingana ili kurahisisha uwekaji wa mbolea.
- Kwa kila sehemu weka kilo moja ya NPK.
- Hii itawezesha utawanyanji sahihi wa mbolea




**Uchanganyaji wa mbolea na odongo**

- Tumia reki au jembe kuingiza mbolea kwenye udongo mbolea iingie sentimenta 1-2 chini ya udongo
- Kwa kutumia jembe utaua magugu ambayo hayatakiwi kuwepo.
- Tumia reki kusawazisha udongo ambao utakuwa umevurugwa na jembe wakati wa kuchanganya mbolea na odongo. Hii itapelekea kupata tuta, ambalo litakuwa tayari kusiw…



**Uchanganyaji wa mbegu na maji**

- Kabla ya kuweka mbegu kwenye keni hakikisha unaweka maji mpaka kwenye mstari kama inavyoonekana kwenye picha. Baada ya kuweka mbegu jaza maji mpaka juu.
- Koroga mchanganyiko wa maji na mbegu kwa kutumia kijiti kabla ya kumwaga kwenye tuta.